



Ilikuwa ni wakati wa likizo. Mboza alisafiri na wazazi wake kwenda kumsalimia bibi yake kijijini. Mboza alikuwa na shauku kubwa ya kumtembelea bibi yake.  
Kila wakati Mboza anapomtembelea bibi yake, bibi humpa zawadi maalum.  
Sijui wakati huu atapewa zawadi gani?

Walipowasili, walimkuta bibi kituo cha basi akiwasubiri.  
Aliwalaki kwa furaha. Mboza alisubiri kwa hamu kujua bibi atampa zawadi gani.  
Alishindwa kusubiri, alimuuliza bibi yake, "Bibi ni zawadi gani sasa utanipa?" Bibi akamwambia awe na subira kidogo hadi wafike nyumbani.



Walipofika nyumbani bibi alitabasamu kisha alisema, "Kipindi hiki sijakuandalia zawadi, utajipa zawadi mwenyewe. Nenda kamkimbize kuku ukimpata ni wako." Bibi alimuonesha Mboza Jogoo.





Mbio zilianza za kumfukuza Jogoo. Loo! Jogoo alikimbia kwa kasi zaidi ya Mboza. Mboza alianguka kwa kishindo puu!

Familia yote ilicheka.  
Jogoo alikimbia zaidi.





Mboza aliamka na kuanza kukimbia tena. Jogoo alikimbilia kwenye kichaka chenye miiba.




“Mboza ni lazima umkamate Jogoo!” Bibi alisema.

Mboza alichukua fimbo. "Koo! Koo!" alisema Jogoo huku akijificha zaidi kichakani.

Mboza alimfukuza, " shiii! shiii! Toka sasa na uanze kukimbia,  
ewe Jogoo mjanja, nitakukamata tu." Alisema Mboza.

Jogoo alipoona fimbo ya Mboza alirukia kwenye mti wa mwembe uliokuwa karibu.







Mboza alipomuona Jogoo juu ya mwembe nae aliamua kupanda kwenye mti wa mwembe akamkamatie huko huko. "Koo! Koo! Koo!" alisema Jogoo.

Tii! Tii! Aligusa gusa maembe. Maembe yalidondoka na kumgonga Mboza kichwani, tii! tii! Mamaa Jogoo anaangusha maembe yananigonga kichwani.



Mboza hakuweza kupanda tena mwembe ule, aliogopa maembe yangemdondokea kichwani. "Koo! Koo!" Jogoo alisema kwa furaha akiwa juu ya mti. Alijua yuko salama. Mboza alimwangalia huku akiwaza, "Nitamkamataje Jogoo huyu?"



“Nitakukamata tu!” Mboza alimwambia Jogoo. Mboza amepata mbinu nyingine. “Nitapanda kwenye mti na hivi vilemba vya bibi.”

Alisema Mboza huku akianua vilemba vya bibi kwenye kamba.



Mboza aliviunganisha vilemba vya bibi.  
Alitengeneza kamba ndefu na imara. Mboza  
aliitumia kamba ile kupanda nayo kwenye mti  
wa mwembe.



“Koo! Koo!” alisema Jogoo. Mboza alipeperusha kamba ile. Waah! ilitoa sauti huku ikimsogelea Jogoo. Jogoo aliogopa mlio wa kamba.



“Koo! Koo!” Jogoo alilia huku akiruka kuelekea chini ya mwembe. Mboza nae huyoo! Akaruka pamoja na Jogoo.



“Bibi,” Mboza aliita. “Nimemkamata Jogoo! Nifanyeje sasa?”





“Sasa tunaweza kumchinja  
na kupika chakula kitamu.”  
Bibi alisema.

“Hatutamchinja leo.” Mboza alisema.  
“Nataka kumpa nafasi Jogoo akimbie,  
nami nimkimbize tena kesho!”





Familia yote walicheka.



